# COMPETENCY BASED CURRICULUM EXAM

PIONEER MARK SERIES

# GREDI YA TANO MWAKA- 2025
# KISWAHILI

**Jina:** ____________________________________________

**Shule:** ____________________ **Nambari ya usajili.** ________ **Tarehe:** ________

## VIWANGO VYA KUZINGATIA KATIKA KUTATHIMINI.

| KUZIDI MATARAJIO | KUFIKIA MATARAJIO | KUKARIBIA MATARAJIO | MBALI NA MATARAJIO | JUMLA (ALAMA %) |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

**Soma mazungumzo yafuatao kisha ujibu maswali yafuatayo**

*(Ni siku ya kwanza shuleni baada ya likizo ya Desemba. Nasu wanakutana na Nimo wakielekea shuleni)*

**Nasu** : Hujambo Nimo?

**Nimo** : (*Akimnyoosheа mkono*) Sijambo Nasu. Habari za likizo?

**Nasu** : Njema labda wewe. Likizo ilikuwa aje?

**Nimo** : (*Kwa furaha*) lo! Nakumbia dadangu likizo yangu ilikuwa na shughuli tele na ziara si haba, sijapataulia hata ng'o! Si harusi, si matanga shughuli zilinibana.

**Nasu** : (Kwa mshangao) Vipi tena?

**Nimo** : (*Akitabasamu*) Ah! Usijali rafiki yangu. Nilizuru ughaibuni kumjulia hali dadayangu. Safari nyingine zilikuwa za humu humu tu. Namshukuru Mungu likizo imekamilika vizuri na tumerudi shule tukiwa wazima wa afya. Je, wewe

**Nasu** : Hmmh...........likizo yangu haikuwa na chochote cha maana. Sikusafiri popote kwani mama yangu hakupata nafasi. Naye nyanya hajapata nafuu

**Nimo** : (*Kwa masikitiko*) Oh! Maskini wamaanisha nyanya bado hajapata afueni baada ya upasuaji? Mola ampe neema zake

**Nasu** : Hata hivyo hatujakata tamaa tuna Imani atapona na kurejelea shughuli zake.

**Maswali**

1. Likizo ya Nimo ilikuwa ya
   A) Ziara na sherehe
   B) Sherehe na kazi nyingi
   C) Ziara, sherehe na shughuli nyinginezo
   D) Kazi nyingi na ziara
2. Ughaibuni ni wapi?
   A) Miji ya mbali
   B) Nchi za mbali
   C) Kwenye starehe nyingi
   D) Miji mikubwa
3. Kipi si kisawe cha neno mungu
   A) Mola
   B) Maulana
   C) Adinasi
   D) Jalali
4. Jibu la maamkuzi sabalkheri ni
   A) Buriani
   B) Inshallah
   C) Aheri
   D) Alamsiki
5. Nimo anajali hali za watu wengine. Chagua kauli anayothibitisha ukweli huu
   A) Anapenda kuwatembelea wagonjwa
   B) Anapenda kuzuru maeneo mbalimbali
   C) Anamcha Mungu
   D) ana uhusiano mwema na dada yake

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali**

Jinsia ni hali ya kike au kiume. Zamani wakati neno usawa lilipokuwa halijapewa umuhimu, watu walikuwa na maoni tofauti kuhusu uana au jinsia na ubinadamu.

Wengine walidhani mtoto wa kike ni bora kuliko wa kiume na wengine walidhani kuwa mtoto wa kiume ni bora zaidi. Siku hizi, mambo yamebadilika na fikra zimebadilika.

Ukweli umepatikana. Ubora wa mtoto ni ubinadamu wake, tabia zake, akili zake na vitendo vyake bora maishani. Si ujinsia. Ubora haufuati ati labda ni mtoto wa kike au wa kiume. Wote ni sawa. Si ajabu kuwa Watoto wa kike wanajua kutekeleza wajibu kwa umakini na kuwajibika zaidi

**Maswali**

**6.** Jinsia maana yake ni hali ya

A) Kike B) Kike au kiume C) Kiume D) Binadamu

**7.** Kwa hakika, ubora wa binadamu hutegemea

A) Ubinadamu na utu B) Pesa C) Jinsia D) Kazi yake

**8.** Ni kauli gani ya kweli kulingana na kifungu?

A) Mtoto wa kike si bora kuliko wa kiume

B) Mtoto wa kiume si bora zaidi kuliko wa kike

C) Ukweli umepatikana kuwa ubora wa mtoto ni tabia zake

D) Ubora wa mtoto si ubinadamu wake

**9.** Katika Habari hii neno jinsia kisawe chake ni

A) Kike B) Kiume C) Uana D) Ubora

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 10 hadi 12**

Tangu zamani mwanadamu amekuwa akijirembesha. Amekuwa akitumia mapambo mbalimbali. Baadhi ya mapambo huvaliwa mikononi kama vile saa, vikuku, pete, na bangili. Mapambo mengine huvaliwa shingoni kama vile mkufu na kidani. Masikioni huvaliwa herini au vipuli. Kwenye miguu huvaliwa vikuku na njuga

Kando na mapambo hayo, kuna yale ya kujipaka pia. Watu hutumia hasa poda na wanja. Poda hupakwa usoni na wanja machoni. Hina hupakwa nyweleni, miguuni, kuchani, na mikononi.

Mtu anapaswa kutumia mapambo haya kwa namna ambayo inafaa. Kutumia mapambo kupita kiasi ni kuharibu urembo; ni sawa na mtu anayetia chumvi nyingi kwenye kitoweo na kukiharibu kikakosa Kulika. Ni muhimu zaidi kutumia mapambo kwa uangalifu mkubwa yasije yakadhuru Ngozi yako.

**10.** Mapambo yamekuwa yakitumiwa hasa kwalengo gani?

A) Kunenepesha mwili B) Kuongeza urembo C) Apite mtihani D) Asifiwe na wenzake

**11.** Nipambo lipi huvaliwa miguuni na mikononi?

A) Pete B) Vikuku C) Bangili D) Mkufu na kidani

**12.** kwa nini mtu anapaswa kuchukua tahadhari anapotumia mapambo?

A) Kila umbo la mtu huhitaji pambo tofauti B) Mengine huwa ya gharama kubwa

C) Baadhi ya mapambo huharibu mwili D) Mengine hudhuru Ngozi

**Swali la 13 hadi 15**

Hapo zamani za kale. Bwana bweha alikuwa na wake na Watoto wengi sana. Siku moja aliamua kuwatembelea wake zake walioishi mbali. Safari hii ilikuwa imepangwa kwa muda mrefu kwani safari yenyewe ingechukua siku kadhaa.

Siku ilipofika, bwana bweha aliamka usiku wa majogoo kuanza safari kabla ya jua kuchomoza. Mwendo ulikuwa mrefu na wa kuchosha kwani mgongoni mwake alibeba zawadi za kuwapelekea wake zake. Bwana bweha alikuwa amefika nusu ya safari yake. Ilimlazimu kutua mzigo wake wa zawadi na kulala ndani ya kichaka

Asubuhi iliyofuata aliamka akiwa na nguvu mpya tayari kuukabili mwendo uliosalia hata ingawa hakula kiamsha kinywa. Alianza safari yake huku akihakikisha kuwa zawadi zake mgongoni zilikuwa salama salimini. Baada ya safari ya siku tatu ya kuvuka milima na mabonde, misitu na nyika,

bwana bweha aliwasili kwa wake zake jioni siku ya tatu.

Alikaribiswa kwa furaha tele. Alionyeshwa chumba cha kupumzika. Bwana bweha aliandaliwa sherehe kubwa. Katika chumba kile alichokuwa akipumzika, harufu tamu ilipenya hadi puani mwake. Hamu ya chakula kile ilimzidi kwani maskini mume wa mtu hakuwa ametia chochote mdomoni kwa siku tatu hivi.

Mgeni alipakuliwa nyama kwenye sinia kisha ikafunikwa kwa kabeji iliyokaangwa. Kutokana na njaa iliyomsokota alikila chakula kwa upesi upesi akashiba. Alipokuwa akichukua kipande cha mwisho ili ajiuzulu, alishtukia pande la nyama lililokaangwa. Alijuta na kusikitika. "laiti ningechakura kabla kula!" lakini alishachelewa.

**13.** Kwa nini safari ya bwana mbweha ilipanga kwa muda mrefu?
A) Alikuwa na Watoto wengi
B) Waka zake waliishi mbali
C) Ilikuwa ya kuwatembelea wake zake
D) Hakuwa amewahi kuwatembelea wake zake

**14.** Unafikiri ni jambo gani ambalo halikufanya safari ya bwana bweha iwe ya kuchosha?
A) Urefu wa safari
B) Zawadi alizobeba mgongoni
C) Ukubwa wa kichaka alimolala
D) Kuchomwa kwa jua kali

**15.** Wenyeji walikuwa wakarimu sana. Ni jambo gani linalothibitisha kauli hii?
A) Walimhurumia mgeni kutokana na safari yake
B) Walimshangilia mgeni wao alipowasili
C) Walimpa mgeni kabeji na nyama
D) Walimpokea mgeni na kumwandalia chakula

**Soma kifungu kifuitacho. Kina nafasi 16 hadi 20 umepewa majibu manne hapo.chagua jibu lifaalo zaidi ya yale uliyopewa.**

Katika gredi________16__________ya tano kuna wanafunzi wengi sana. Gredi hii______17______na kiranja____18____hutekeleza________19__________yake bila upendeleo Mwalimu aondokapo darasani. Je __________20__________kiranja huyu hufanikiwa namna gani.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 16. | A) chetu | B) Mwetu | C) Letu | D) Yetu |
| 17. | A) Imesimamika | B) Imesimamisha | C) Limesimamiwa | D) Imesimamiwa |
| 18. | A) Ambae | B) Ambalo | C) Ambaye | D) Ambawo |
| 19. | A) Majukumu | B) Wajibu | C) Majibu | D) Sera |
| 20. | A) ? | B) , | C) ! | D) ; |

**Chagua jibu sahihi**

**21.** Kamilisha methali hii
Mtoto umleavyo ndivyo
A) Ako B) Atakuona C) Akuavyo D) Huwa

**22.** Kamilisha kitendawili hiki
Chakula kikuu cha mtoto
A) Yai B) Usingizi C) Maziwa D) Ndizi

**23.** Chagua nomino makundi kukamilisha pengo
Tunasema thurea ya__________
A) Nyota B) Nguo C) Shule D) Kuni

**24.** Ambatanisha maagano na jibu lake
Alamsiki
A) Aheri
B) Binuri
C) Sabalheri
D) Njema

**25.** Pete nipambo linalovaliwa kwenye kidole. Je, pambo gani linalovaliwa kwenye shingo?
A) Taji
B) Mkufu
C) Chupio
D) Kipuli

**26.** Abel ni mtulivu kama maji mtungini. Moni naye ni mjanja kama
A) Kobe B) Kinyonga C) Sungura D) Ndege

**27.** Chagua vihisishi katika sentensi
Lakini, pia, oyee!, mwema, ingawa, laiti!, ndani ya
A) Mwema, laiti
B) Ndani ya, ingawa
C) Pia, oyee!
D) Oyee!, laiti!

**28.** Maana ya nahau "piga deki" ni
A) Kufua
B) Kupanga
C) Kuosha
D) Kucheza

**29.** Panga maneno haya kulingana na kamusi
Sita, sahani, shimo, sehemu
A) Sahani, sehemu, shimo, sita
B) Sita, shimo, sehemu, Sahani
C) Sehemu, shimo, Sahani, sita
D) Sahani, shimo, Sahani, sita

**30.** ____________ Ni mtu anayeimba shairi
A) Mwimbaji
B) Sogora
C) Manju
D) Mtunzi

## INSHA (alama 20)

**Mwandikie rafiki yako barua ukimwalika kusherehekea siku ya kuzaliwa kwako.**

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................